Sasisho la COVID-19 ya Jiji la Burlington

Kituo cha Rasilimali na Kupona kwa COVID-19 cha Burlington (RRC)

Mei 2021

Kiswahili

Maangazio:

- Mpango wa Vermont wa Baadaye - Mwongozo wa Kufungua Tena
- Hali ya Kisa cha COVID-19
- Miongozo Iliyosishwa kuhusu Barakoa
- Mkakati wa Mafunzo ya Mapema - Mpango wa Ufadhili wa Masomo kwa Utunzaji wa Mtoto
- VERAP - Mpango wa Usaidizi wa Dharura ya Kodi ya Nyumba katika Vermont
- Kuendelea, Kupiga Hatua - Mpango wa mafunzo ya kazi ya Msaidizi wa Muuguzi Aliye na Leseni (LNA)

Mpango wa Vermont wa Baadaye



"Mpango wa Vermont wa Baadaye", ulitangazwa hivi karibuni ambao utaendelea na kuleta athari katika miezi ijayo. Lengo ni kufunguliwa tena kwa shughuli zote kufika tarehe 4 mwezi wa Julai. Mpango huu unatoa mwongozo wa kufunguliwa tena ili kuwasaidia wakazi wa Vermont na biashara za ndani kuona njia ya baadaye kwa kurejeshwa kwa usafiri usio na vikwazo, uendeshaji wa biashara, na mikusanyiko ya matukio. Mpango huo uliundwa na Idara ya Afya, Idara ya Usalama wa Umma, na Shirika la Biashara na Maendeleo ya Jumuiya na hutumia data ya chanjo kuhakikisha kufunguliwa upya kwa jimbo salama.

Visasisho Muhimu vinajumuisha:

Mei tarehe 14 - **Kisasisho cha Mkusanyiko wa Watu** - Ikiwa tukio halina njia ya kujua ikiwa mtu amepewa chanjo, chukulia kuwa wote hawajapewa chanjo kwa kipimo cha nafasi. Matukio na mikutano lazima ifuate Mwongozo wa Ulimwenguni (katika Kiingereza), **inayojumuisha mahitaji ya kukaa mbali na wengine na kuvaa barakoa.**

- **Kipimo cha Mikutano ya Ndani ya Nyumba:** Mtu mmoja asiyepewa chanjo kwa kila futi mraba 50 hadi watu 300 ambao hawajapokea chanjo (yoyote iliyo kidogo), pamoja na idadi yoyote ya watu waliopewa chanjo jinsi ambavyo Mwongozo wa uwekaji nafasi kote Ulimwenguni unaruhusu.
- **Kipimo cha Mikutano ya Nje ya Nyumba:** Hadi watu 900 ambao hawajapokea chanjo, pamoja na idadi yoyote ya watu waliopewa chanjo jinsi ambavyo Mwongozo wa uwekaji nafasi kote Ulimwenguni unaruhusu.

Vizuizi vya Usafiri Vimeondolewa – Karantini na kipimo havihitajiki tena kwa ajili ya usafiri unaporejea Vermont. Hata hivyo, vizuizi fulani vya karantini na kipimo bado vinaweza kutumika katika usafiri wa kimataifa. Mwongozo unaweza kutofautiana kutegemea jimbo, hivyo kabla ya kuratibu ziara, angalia mwongozo wa usafiri wa ufikio wako.

Julai tarehe 4 - **Vizuizi Vyote Vimeondolewa**

- Mikutano na matukio - hakuna vizuizi vya idadi, matukio ya nje ya nyumba yanahimizwa
- Mahitaji ya barakoa na kukaa mbali na wengine - hayahitajiki lakini yanahimizwa sana
- Uendeshaji wa Biashara - Mwongozo wa Ulimwenguni (katika Kiingereza) unahimizwa kwa sekta zote

Hali ya Kisa cha COVID-19



Jiji linaendelea kufuatilia uwepo wa COVID-19 katika jumuiya**. Ripoti za hivi karibuni zinaonyesha kuwa kuna ongezeko la visa katika ukanda wetu, kufikia mwisho wa Aprili.**

- Wastani wa siku saba (kufikia mwisho wa Aprili) - visa 21.6 vilivyoripotiwa.
- Kikundi kikubwa cha umri ambacho kinapatikana na COVID-19 (katika wiki 4 zilizopita) - umri wa miaka 20-29.
- Data ya hivi karibuni inaonyesha kuwa **zaidi ya 61% ya wanachama wa jumuiya ya Vermont wamepokea angalau dozi moja ya chanjo.**
- Visa vya COVID-19 vinavyohusiana na watu wazee katika jumuiya vinapungua kwa sababu wengi wanachukua fursa ya chanjo**. Huku iddi hizi zinaonyesha hatua nzuri, bado tunahitaji kuendelea kuwa waangalifu kwa wakati huu.**

<u>Unachoweza kufanya:</u> Tafadhali endelea kuvaa barakoa, fuata mwongozo wa Jimbo kuhusu kukusanyika na watu wasio wa kaya yako, na kuzingatia kipimo cha bila malipo (ambacho ni sampuli ya pua lako kwa njia rahisi na kujifanyia, si kipimo cha awali kilichoenda zaidi katika nyuma ya pua lako) kinachopatikana katika 405 Pine Street katika Burlington kila siku kati ya saa 4:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni. Kupata chanjo pia kunaweza kupunguza kwa kikubwa msambao wa virusi ndani ya jumuiya.

Mkakati wa Mafunzo ya Mapema

first steps Scholarship Program



Je, unahitaji usaidizi wa kulipia utunzaji wa mtoto? Mtoto wako anaweza kufuzu kwa Mpango wa Ufadhili wa Masomo wa Hatua za Kwanza

Familia zinazostahiki zinaweza kupokea ***Ufadhili wa Masomo wa Hatua za Kwanza*** kupitia Jiji la Burlington, ili kusaidia kwa gharama za masomo kwa utunzaji mtoto wa muda wote katika mipango iliyofuzu! Kuomba, familia zinahitaji kuwa wakazi wa Burlington, wanatimiza miongozo ya mapato inayofuata, na wana mtoto aliye na umri wa wiki 8 hadi miaka 2 ½. Tumia kiungo ili kupata maelezo zaidi!

Mapato ya familia ya kaya lazima yawe sawa na au chini ya 80% ya Mapato ya Wastani ya Eneo hilo (AMI).

Ukubwa wa Kaya	watu 2	watu 3	watu 4	watu 5	watu 6	watu 7	watu 8
Mapato ya Kila Mwaka ni sawa na au chini ya	$61,400	69,050	$76,700	$82,850	$89,900	$95,150	$101,250

JINSI YA KUTUMA OMBI:
Maombi yanakubaliwa kwa kipindi cha kutuma maombi ya ufadhili wa masomo cha 2020–2021. Kutuma ombi, piga simu au tuma barua pepe kwa Paula Bonnie kupitia paula@letsgrowkids.org au 802-398-5464. Pia unaweza kuwasiliana na Kituo cha Simu cha RRC kupitia 802-755-7239 ili kupata usaidizi. Mkalimani kupitia kwa simu ya mkononi zinapatikana.

Jifunze zaidi katika www.burlingtonvt.gov/it/earlylearning.

Mpango wa Usaidizi wa Dharura ya Kodi ya Nyumba katika Vermont

Mpango wa Usaidizi wa Dharura ya Kodi ya Nyumba katika Vermont uliundwa ili **kusaidia wakodishaji wanaokabiliana na changamoto za kifedha zinazohusiana na janga la COVID-19**. Kwa kaya zinazofuzu, mpango huo unatoa kodi na usaidizi wa matumizi ili kuwasaidia wakazi wa Vermont kuepuka kuondolewa kwa nyumba au kupoteza huduma ya matumizi.

Mpango huo husaidia kaya kwa kulipa **salio za kodi za sasa na zilizopita, matumizi na gharama za kawi ya nyumbani ya sasa na zilizopita, na matumizi mengine yanayohusiana na nyumba**. Usaidizi wa matumizi unaweza kujumuisha umeme, gesi, maji, taka, kuondolewa kwa takataka na gharama za kawi, kama vile mafuta. Maombi yatahitaji kukamislishwa na mkodishaji na mmiliki wa mali hiyo, na malipo ya moja kwa moja yatafanywa kwa mmiliki.

Tovuti: https://erap.vsha.org/ (katika Kiingereza)

Kwa ajili ya Usaidizi wa Maombi na Msaada wa Lugha, wasiliana na:

AALV - Muungano wa Waafrika Wanaoishi katika Vermont
http://www.aalv-vt.org/
(802) 985-3106

CVOEO - Mradi wa Uwezeshaji wa Kifedha kwa Wamarekani Wapya
https://www.cvoeo.org/
(802) 860-1417 x117

USCRI Vermont - Kamati ya Marekani ya Wakimbizi na Wahamiaji
https://refugees.org/uscri-vermont/
(802) 655-1963

Kuendelea, Kupiga Hatua

UKO TAYARI KWA MABADILIKO?
Anza KAZI MPYA katika huduma ya afya na KUPIGA HATUA!

Pata MAPATO YA JUU kama Msaidizi wa Muuguzi Aliye na Leseni (LNA). Mpango huu wa mafunzo ya LNA utawapa washiriki:

- Kozi ya wiki 10 inayotolewa mtandaoni na kwa mtu binafsi
- Saa 32 za mafunzo halisi YENYE MALIPO, baada ya kukamilisha kozi
- Maandalizi kamili ya Mtihani wa Msalaba Mwekundu wa Utoaji Leseni ya LNA
- Ukuaji kitaaluma
- Kuendelea, Kupiga Hatua inashirikiana na UVMMC, Ethan Allen Residence na Cathedral Square
- Hakuna malipo kwa waombaji wote watakaofuzu

Ratiba:
Kazi za kozi ni usiku tatu kwa wiki, saa 12:00 jioni hadi saa 3:00 usiku.

Kutuma Ombi:
Tembelea www.burlingtonvt.gov/covid-19/LNA
Kwa maswali, tuma barua pepe kwa CEDOLNA@burlingtonvt.gov.
Maombi yatakaguliwa kwa msingi unaoendelea kuanzia Mei tarehe 10.

Taarifa ya COVID-19

Idara ya Afya ya Vermont ina kurasa za lugha maalum zenye maelezo ya afya ya COVID-19:

Kiswahili: https://www.healthvermont.gov/covid-19/resources/multilingual-resources#Swahili

Maswali? Je, Unahitaji Usaidizi?

Kituo cha Rasilimali na Kupona kwa COVID-19 cha Burlington kiko hapa kukusaidia, wasiliana nasi kupitia 802-755-7239 au recovery@burlingtonvt.gov na uache ujumbe wenye jina lako, lugha unayopendelea, na maelezo ya mawasiliano na tutakusaidia haraka iwezekanavyo. Kituo chetu cha kupokea simu kina huduma za ukalimani kwa simu. Saa zetu za kufanya kazi ni Jumatatu hadi Ijumaa, 2:00 asubuhi hadi 10:30 jioni.

Pata Tafsiri:

Idara ya Afya ya Vermont
https://www.healthvermont.gov/media/translation/covid-19-translations
Jiji la Burlington
https://www.burlingtonvt.gov/covid-19/translated
Jopo Kazi la Lugha Anuwai katika Vermont:
https://www.youtube.com/channel/UC3zjPpeFnXqvESr1y3d4DvQ

Taarifa katika waraka huu inaweza kubadilika jinsi miongozo inasasishwa katika kiwango cha kitaifa na jimbo